**Eldad Jeremia Mulwambo, (1948–2013)**

Eldad Jeremia Mulwambo, alikuwa mhudumu, mwalimu, mwinjilisti, mpanda makanisa, na msimamizi wa kazi nchini Tanzania.

**Maisha ya siku za awali:**

Eldad Jeremia Mulwambo alizaliwa mwaka 1948 katika Kisiwa cha Ukerewe, Mkoa wa Mwanza, nchini Tanzania. Wazazi wake wote wawili, Jeremia Mulwambo Sakara na Perusi, walikuwa wenyeji wa Ukerewe na Waadventista wa Sabato waliojitoa sana kwa kazi. Waliongokea kwenye Uadventista baada ya mafundisho ya Waadventista kuletwa kijijini kwao na wamishionari wenyeji kutoka Majita. Baba yake, mzee Jeremia Mulwambo alikuwa na watoto tisa: wavulana watatu na wasichana sita ambapo Eldadi Mulwambo alikuwa mtoto wa pili kuzaliwa kwenye familia yao. Inadaiwa kuwa baba yake mzee Jeremia Mulwambo aliishi maisha ya kielelezo yaliyojenga msingi thabiti katika kumwogopa Mungu kwa watu wa familia yake na majirani zake wengine.

**Elimu:**

Eldad Mulwambo alipata elimu yake ya msingi katika Shule ya Kati ya Tangaza. Baada ya hapo, alienda kwa elimu ya sekondari nchini Uganda. Ingawa shule hizi hazikuwa za Waadventista, imani ya Eldad Mulwambo iliendelea kuimarika licha ya changamoto kadhaa alizokumbana nazo katika shule hizo. Kutokea wakati huo, Eldad alihudhuria Chuo cha Waadventista cha Ikizu mnamo 1975, ambapo alipata mafunzo ya uchungaji. Mchungaji Mulwambo aliendelea kupambania elimu na maendeleo yake bila kukata tamaa. Kutokana na shauku yake ya kuwa na elimu ya juu, Jeremia Mulwambo alihudhuria Chuo cha Kiadventista cha Memorial Spicer nchini India ambako alihitimu shahada yake ya kwanza ya theolojia. Mara tu baada ya kuhitimu shahada hiyo mwaka wa 1984, alijiunga na shahada ya uzamili akijikita katika kusomea historia kwenye Chuo Kikuu cha Poona na baadaye shahada ya uzamili katika sosholojia katika Taasisi za Kijamii za Nehru nchini India.

Mafanikio yake ya kielimu yaliwatia moyo wahudumu vijana wa siku zake, kama vile Mchungaji Herry Muhando na Mchungaji Jacob Gagi, kujiendeleza kwa masomo ya juu. Ikumbukwe kwamba wakati huo, kanisa barani Afrika lilikuwa na Waafrika wachache wenye elimu ya uzamili.

**Uchungaji wa Mapema:**

Mchungaji Jeremia Mulwambo alijiunga na huduma ya kichungaji katika Kanisa la Waadventista wa Sabato mwaka 1972 akiwa mwinjilisti wa vitabu wilayani Ukerewe. Alifurahia kufanya kazi hiyo hadi alipoitwa kuwa mchungaji wa mtaa wa Kisoria wilayani Bunda mkoani Mara. Wakati huo, Mchungaji Jeremia Mulwambo alijishughulisha na uinjilisti na upandaji wa makanisa. Alikuwa mchungaji kijana mwenye maono na shauku ya uchungaji. Alijitolea kumtumikia Mungu na kanisa lake.

Baada ya kazi kubwa aliyoifanya Ukerewe na Mkoa wa Mara, Mchungaji Mulwambo alihamishiwa Shule ya Sekondari ya Parane na kuwa Mlezi wa kiroho wa shule yaani Chaplain. Alihudumu kama Chaplain kuanzia 1976 hadi 1979. Akielezea huduma ya Mchungaji Mulwambo huko Parane, Mchungaji Jacob Gagi, ambaye pia alifundisha katika shule hiyo, anasema Mulwambo alikuwa mchungaji mwenye bidii. Alichanganyika na wanafunzi katika shughuli mbalimbali, kama vile kulima na kukusanya kuni na kuzikata huko msituni. Wakati wa uchungaji wake katika Shule ya Sekondari ya Parane, roho yake ya uinjilisti iliwashwa. Katika kipindi cha miaka minne akiwa shuleni hapo, aliendesha mikutano miwili ya hadhara ya uinjilisti iliyokuwa inafahamika kama effort. Tangu wakati huo, Parane haijaacha kufanya mikutano hiyo ya uinjilisti. Baada ya elimu yake nchini India, Mchungaji Mulwambo alihudumu tena huko Parane kuanzia 1986 hadi Desemba 1988.

**Ndoa na Familia:**

Mchungaji Mulwambo alimuoa Lucy Nyabweke Murusuri mnamo 1976. Walienda pamoja kama timu katika huduma wakitokea Kisoria hadi Parane, na kutoka India kurudi Parane kwa miaka miwili. Baada ya hapo walihamia sehemu mbalimbali zikiwemo Arusha, Morogoro, Kigoma, Dar es Salaam na hatimaye kurudi Morogoro kwenye makazi yao ya kustaafia ambako umauti ulimkuta. Mchungaji Eldad Jeremia Mulwambo alizikwa hapo Morogoro akisubiri ahadi ya ujio wa pili wa Bwana.

**Mchango wa Mama Mulwambo**

Bibi Mulwambo alifanya kazi katika nyadhifa mbalimbali katika Kanisa la Waadventista wa Sabato. Akiwa Parane, alifanya kazi kama mwalimu. Katika Seminari na Chuo cha Waadventista wa Sabato Tanzania, alifanya kazi kama mwalimu na meneja wa mgahawa. Katika Fildi ya Tanzania Mashariki ya wakati huo, alikuwa katibu muhtasi wa ofisi ya makao makuu ya Fildi. Pia alikuwa mkurugenzi wa Huduma za Wanawake na Watoto katika Fildi ya West Tanzania. Alikuwa mchapakazi, mshauri wa Mchungaji Mulwambo. Alikuwa mama mwenye upendo kwa watoto wao watano, mwalimu, na mwangalizi katika shamba la mizabibu la Mungu. Mchango wake kwa Kanisa la Waadventista hautasahaulika kamwe. Bibi Mulwambo alilala katika Bwana Aprili 23, 2017. Alizikwa katika makaburi ya Mlima Kora kwenye manispaa ya Morogoro.

**Watoto wao:**

Mchungaji Mulwambo na mkewe Lucy walijaliwa watoto watano, wavulana wawili na wasichana watatu: Mark, Mugara, Maradufu, Maria, na Mwasi. Watoto wa Mchungaji Mulwambo wanamkumbuka baba yao kama baba mwenye upendo na anayejali licha ya kuwa na shughuli nyingi za kiutawala. Kila mara alipata muda na watoto wake, kwa kuwashauri na kwa mafunzo, na alikuwa shujaa kwao.

**Majukumu ya Utawala**

Safari ya uongozi ya Mchungaji Mulwambo ilianza mwaka 1988 alipoitwa kuwa mkuu wa Tanzania Adventist Seminary and College Arusha (TASC). Katika mwaka huo huo, aliwekewa mikono ya kichungaji na kuwa mhudumu wa injili katika Kanisa la Waadventista. Wakati akiwa mkuu wa shule, seminari hiyo iliongeza kozi mbali mbali kando ya ile ya mafunzo ya uchungaji, kama vile cheti cha huduma za ukatibu, diploma ya usimamizi wa biashara, na diploma ya elimu. Mbali na maendeleo hayo ya kitaaluma, baadhi ya miundombinu ilianzishwa, ikiwa ni pamoja na mabweni ya wanawake na wanaume na nyumba moja ya wafanyakazi. Kutokana na awamu hii ya maendeleo, Tanzania Adventist Seminary and College ilianza safari iliyochangia kusajiliwa kwake kama Chuo Kikuu cha Arusha.

Mwaka 1991 Mchungaji Mulwambo aliitwa kuhudumu kama Mwenyekiti wa Fildi ya Tanzania Mashariki, yenye makao yake makuu mjini Morogoro. Kufikia wakati huo, Fildi hiyo ilikuwa ikijumuisha mikoa ya kiutawala ya serikali ya Mtwara, Lindi, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, na visiwa vya Unguja na Pemba na Visiwa vya Zanzibar. Wakati huu, kazi ya umishionari ya Waadventista ilikuwa bado katika hatua za mwanzo katika sehemu nyingi za maeneo hayo. Mchungaji Manento anaelezea miaka hii kama miaka ya taabu, jasho na joto. Kulikuwa na uhaba wa rasilimali fedha na watu. Pamoja na changamoto zote hizo, Kanisa hilo katika Fildi ya Tanzania Mashariki lilifanikiwa kuanzisha zahanati katika Kisiwa cha Pemba ambacho kina Waislamu wengi.

Wakati wa kikao cha uchaguzi cha Union kilichofanyika kuelekea mwisho wa mwaka wa 2000, Mchungaji Mulwambo alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Fildi ya Magharibi mwa Tanzania. Fildi ya Magharibi mwa Tanzania ulihusisha mikoa ya utawala ya serikali ya Kigoma, Kagera, Tabora, Singida na Wilaya ya Mpanda, ambayo wakati huo ilikuwa katika mkoa wa utawala wa Rukwa. Siku hizo, kusafiri kwa barabara lilikuwa jambo la hatari sana. Lakini Mchungaji Mulwambo alisafiri katika eneo la West Tanzania Field bila woga. Mchungaji Mngwabi, ambaye aliwahi kufanya kazi naye West Tanzania Field, alitoa ushuhuda kuhusu namna alivyokuwa mmoja wa abiria wake pale majambazi wenye silaha walipowavamia na kutishia kuwaua walipokuwa wakisafiri kwenda kutembelea makanisa. Lakini Mungu alikuwa mwema, kwani Mchungaji Mulwambo na aliokuwa nao walisalimika na hawakudhurika kabisa.

Akiwa Mwenyekiti wa West Tanzania Field, Mchungaji Mulwambo na timu yake walianza kujenga jengo jipya la ofisi. Mradi huu ulianzishwa kwa imani kwa sababu hapakuwa na fedha. Lakini alifaulu kuwahamasisha waumini, nao wakaanza kujenga jengo jipya. Kufikia mwisho wa 2005, jengo la ofisi, ingawa lilikuwa halijakamilika kabisa, lilikuwa na vyumba vya kutosha kuruhusu wafanyakazi wote wa West Tanzania Field watumie kama mahali pao papya pa kufanyia kazi.

Mchungaji Mulwambo alipata fursa adimu ya kuwa mjumbe wa Kikao cha Konferensi Kuu ya Ulimwengu cha 2005 ambacho kilifanyika huko Saint Louis, Missouri, Marekani. Zaidi ya hayo, Mchungaji Mulwambo alihudumu katika Halmashauri Kuu ya Union ya Tanzania kwa miaka 21 mfululizo. Hili liliwezekana kwa sababu, kwa miaka hiyo yote, aliwahi kuwa Mwenyekiti wa fildi fulani au mkuu wa taasisi ya union. Kulingana na taratibu za kanisa, na nyadhifa zote mbili zilimstahilisha kuwa mshiriki wa vikao vya Union.

Akiwa mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Union ya Tanzania, alihudumu pamoja na wenyeviti wa Union wafuatao: Dk. Robert Taylor, Mchungaji Yohana Lusingu, Mchungaji Lameck Mwamukonda, Mchungaji Geoffrey Mbwana, Mchungaji Magesa Bina, na Mchungaji Joshua Kajula. Pia alifanya kazi kwa karibu na Mzee Eliamani Kachua, Meneja Biashara wa Tanzania Adventist Seminary and College; Mchungaji Mangi Fadhili Manento, Katibu na Mwekahazina wa Fildi ya Tanzania Mashariki; Bwana Mathias Mavanza, Katibu na Mwekahazina wa Fildi ya Tanzania Mashariki; Mzee Julius Rulanyaga, Katibu na Mwekahazina wa Fildi ya Magharibi mwa Tanzania; Mchungaji Joseph Mngwabi, Katibu wa West Tanzania Field; na Denis Wairaha, Mwekahazina wa Fildi ya Magharibi mwa Tanzania.

**Miaka ya Baadaye ya Huduma na Mauti**

Baada ya kuhudumu kama Mwenyekiti wa West Tanzania Field (2001–2010), Mchungaji Mulwambo aliitwa kuhudumu kama mchungaji wa mtaa wa Ilala jijini Dar es Salaam mwaka 2011. Kufikia wakati huu, Wilaya ya Ilala ilikuwa na makanisa manne, likiwemo kanisa la Mzizima, ambalo halikuwa na jengo la ibada la kudumu. Mchungaji Mulwambo aliona kuwahudumia waumini wa kanisa hili ni changamoto ya kipekee. Waumini wa kanisa hili walijumuisha wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili, Chuo cha Ufundi Dar es Salaam, na Taasisi ya Usimamizi wa Fedha pamoja na waumini wa kawaida wa kanisa waliotoka katika maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam.

Kabla ya kulala katika Bwana, Mchungaji Mulwambo alihamishiwa Morogoro, Mtaa wa Misufini, ambako alichunga makanisa sita. Miaka yake ya mwisho ya huduma ilijaa tumaini la kurudi kwa Kristo upesi. Alilala katika Bwana mnamo Septemba 26, 2013.

**Urithi Aliotuachia:**

Mchungaji Eldad Jeremia Mulwambo atakumbukwa kwa ucheshi wake, uchapakazi, usimamizi mzuri, na kujitoa katika uinjilisti na moyo wa upandaji wa makanisa.